

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
Ofisi ya Rais
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Telegrams: MKUU WA WILAYA

Telephone: 0732-988332

Fax; 0732-988484

Email: dc.urambo@tabora.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
30 Barabara ya Boma-Stendi
S. L. P. 83,
45582 URAMBO, TABORA.

KUMB. NA. AB.15/60/01/49

Tarehe: 30/09/2024

TANGAZO

WANANCHI WOTE,
WILAYA YA URAMBO.

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA VIJANA WA KUJIUNGA NA JESHI LA KUJENGA
TAIFA (JKT) KWA MWAKA 2024/2025.

Tafadhali rejeeni kichwa cha bahari hapo Juu,

02. Jeshi la kujenga Taifa (JKT) litaandikisha vijana wa kujitolea kwa hiari kutoka Vijijini na Mjini kwa mkataba wa miaka miwili ya kulitumikia Taifa.
03. Katika hali hiyo Vijiji watakapotoka vijana hao vitaweza kupata fursa ya kutumia ujuzi wao watakaporudi vijijini baada ya kumaliza muda wao wa kulitumikia Taifa na kujifunza stadi mbalimbali za kazi.

Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;-

04. SIFA ZA WAOMBAJI:


1. Awe ni raia wa Tanzania
2. Umri
 - a. Vijana wenye Elimu ya darasa la saba umri ni kuanzia miaka **16** hadi **18**,awe amemaliza Elimu ya msingi kuanzia Mwaka **2021,2022,na 2023** awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Msingi.
 - b. Vijana wenye Elimu ya Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka **20**,waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka **2021,2022,2023** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate).Awe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi la nne. Awe na ufaulu wa alama kuanzia **26** hadi **32**.
 - c. Vijana wenye Elimu ya Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka **22** waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia **2021,2022,2023** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate).Awe na ufaulu wa kuanzia daraja la kwanza hadi la Nne.
 - d. Vijana wenye Elimu ya Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka **25**,Awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
 - e. Vijana wenye Elimu ya Shahada umri usiwe zaidi ya miaka **26**,Awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
 - f. Vijana wenye Elimu ya Shahada ya Uzamili umri usiwe zaidi ya miaka **27**,Awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo
3. Awe na Afya njema ,Akili timamu na asiwe na Alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo).
4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia mahakamani na hajawahi kufungwa.
5. Awe na Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA)
6. Awe na cheti cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).
7. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi maalumu cha kuzuia Magendo wala kuajiriwa na Idara nyingine Serikalini.

8. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma kwa kundi la kujitolea na kundi la lazima (Mujibu wa Sheria).
9. Asiwe anajihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.
10. **Angalizo** : Kijana atakayepatikana na nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua kali za kisheria kulingana na taratibu zilizopo.

05. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI.

NB: Maombi yatumwe kwa **KATIBU TAWALA WILAYA, S.L.P 83, URAMBO.** Kupitia kwa Afisa Mtendaji wa Kata husika.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 07/10/2024 saa 9:30 mchana na Usaili (interview) utafanyika tarehe 08/10/2024 saa 2:00 asubuhi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Urambo.


Innocent M. Nsena
Katibu Tawala Wilaya
URAMBO.
KATIBU TAWALA WA WILAYA
URAMBO

Nakala : Mkuu wa Wilaya
URAMBO - Aione kwenye jalada

Mshauri wa Jeshi la Akiba (W)
URAMBO-Kwa taarifa na Uratibu

Maafisa Tarafa,
USSOKE NA URAMBO

Watendaji wa Kata,
WILAYA YA URAMBO.

Mbao zote za Matangazo
URAMBO.